

MAMLAKA YA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI



28/07/2022

TANGAZO LA MNADA WA MAGARI

Wananchi wote mnatangaziwa kuwa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) itauza kwa njia ya Mnada wa hadhara jumla ya magari mawili (2) Nissan D/C. Mnada wa magari utafanyika tarehe 13/08/2022 Ofisi za Mamlaka zilizoko barabara ya 05 Barack Obama jirani na Taasisi ya Saratani Ocean Road kuanzia saa 4.00 asubuhi.

MASHARTI YA MNADA

1. Mnunuzi atalazimika kulipa papo hapo amana (deposit) isiyopungua asilimia **Ishirini na Tano (25%)** ya thamani ya gari atakayonunua, na kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi na nne(14) kuanzia tarehe ya mnada kufanyika. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa kemikali na magari na amana iliyolipwa **haitarudishwa**.
2. Mnunuzi atatakiwa kuondoa/kuchukua mali aliyonunua katika muda wa siku saba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
3. Ruhusa ya kuangalia/ kukagua magari itatolewa siku mbili (2) kabla ya tarehe ya kufanyika mnada husika kwa saa za kazi.
4. Mnada utanza saa Nne (04.00) asubuhi katika ofisi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Makao Makuu Dar es Salaam barabara ya 05 Barack Obama jirani na Taasisi ya Saratani Ocean Road.
5. **Imetolewa na;**

Sylvester Omary

Msimamizi wa Kitengo Cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma.